(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Tel. 028280 4865
Fax. 028280 2719/2370
Email: ded@Kigomadc.Go.Tz

KIGOMA DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 332

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P. 332,
Kigoma.

Kumb.Na.KDC/C.1/36/102 Tarehe: 21 Februari, 2021

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma anapenda kuwatangazia Watanzania wote kuwa ofisi ya Rais-UTUMISHI imetoa kibali cha ajira ch ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/358/01"C"/98 cha tarehe 24 Januari,2022 kwa ajili ya kutangaza nafasi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III kwaMasharti ya kudumu.Hivyo Watanzania wote wenye sifa mnaombwa kuomba nafasi hiyo kama ifuatavyo;
:

## 1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III NAFASI (01)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango yamaendeleo ya Kijiji.
iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
v. Kutafsirina kusimamia sera, sheria na taratibu.
vi. Kundaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kusimamia Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
vii. Kiongozi na Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
viii. Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
ix. Kupokea,kusikiliza na kutatua malalamiko ya wanachi.
x. Kusimamia Utungaji wa sheria ndogo ndogo za kijiji.
xi. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika kijiji.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Mtanzania.
ii. Awe na Elimu Kidato cha Nne au cha Sita.
iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (NTA Level 5) katika moja ya Fani za Utawala, sheria, Maendeleo, Elimu ya Jamii na Sayansi ya Sanaa,

Usimamizi wa Fedha kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo – Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

iv. Awe na umri wa Miaka 18 au zaidi na asiwe na umri usiozidi miaka 45.

v. Awe na Afya njema, Mchapakazi, na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote katika Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kgoma.

vi. Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).

## 2.0 UTARATIBU WA KUOMBA

a. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma **S.L.P 332 KIGOMA.**

b. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya Taaluma na vya Mafunzo pia cheti cha kuzaliwa na vyeti vithibitishwe.

c. Testimonials "Provisional Results; Statement of Results; hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI.**

d. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika yaani **TCU** na **NECTA.**

**2.1.** Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe tarehe 07.03.2022
Maombi yote yatumwe kwa

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**S.L.P.332,**
**KIGOMA.**

Tangazo hili limetolewa na

Archard Joseph Bajumuzi
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA